

## Kura ya Maoni ya Sauti ya Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait

Hivi karibuni wapigaji kura wa Australia wataombwa kupiga kura katika Kura ya Maoni. Kura ya Maoni itauliza ikiwa ni muhimu kuwepo Sauti ya Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait kwenye Bunge katika Katiba. Bunge ndicho chombo kinachotunga sheria kwa ajili ya Australia.

### Sauti kwa Bunge ni nini?

Sauti ni njia ambayo Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait wanaweza kuishauri Serikali kuhusu sheria zinazowahu. Kuandika Sauti katika Katiba kutamaanisha Sauti itakuwa na kazi ya kudumu ya kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu masuala yanayohusu Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait. Sauti kwa Bunge itakuwa fursa kwa Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait kutambuliwa kikatiba na kwa tamaduni zao kutambuliwa na kusherehekewa.

### Kwa nini Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait wanaomba kuwa na Sauti kwa Bunge?

Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait wamekuwa wanaomba kutambuliwa na Serikali kwa karibu muda wa miaka 100. Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait hujua jumuiya zao na tamaduni zao vizuri sana. Wanajua suluhu bora za kukubaliana na changamoto za jumuiya zao ambazo zinaweza kuunda uzoefu wenye haki na usawa zaidi kwa Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait.

### Sauti kwa Bunge itafanya nini?

Sauti itasikiliza ushauri kutoka Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait kuhusu masuala yanayohusu maisha yao, ili Serikali iweze kufanya maamuzi mazuri zaidi yanayoathiri Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait.

### Nani watawakilisha Sauti kwa Bunge?

Sauti itakuwa kikundi cha Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait kutoka kila jimbo na wilaya ikiwa ni pamoja na maeneo ya mbali. Wawakilishi watachaguliwa na Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait katika maeneo yao ya mitaa.

### Je, Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait wameshauriwa kuhusu Sauti kwa Bunge?

Maelfu ya Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait wametoa ushauri kuhusu kwa nini Sauti inahitajika na jinsi inavyopaswa kufanya kazi kwa miaka mingi. Zaidi ya 80% ya Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait wanaunga mkono na Sauti kwa Bunge.

### Wataalamu wa kisheria wanasemajie?

Wanasheria wa katiba wakiwemo wale ambao wanawakilisha Serikali ya Shirikisho wamesema Sauti ni halali kisheria na itafanya mfumo wetu wa serikali uwe mzuri zaidi.

### Je, Sauti inaweza kutengeneza sheria?

Hapana. Sauti haitakuwa na mamlaka kutunga sheria. Itatoa ushauri tu kuhusu masuala yanayowahu. Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait.

### Kura ya Maoni ya Sauti ya Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait itauliza swali gani?

“Sheria Iliyopendekezwa: kubadilisha Katiba ili kutambua Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait wa Australia kwa kuanzisha Sauti ya Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait. Je, unakubali mabadiliko yaliyopendekezwa?”

### Je, nitapiga kura jinsi gani katika Kura ya Maoni?

Kura za maoni ni kama uchaguzi. Utapewa karatasi ya kupigia kura pamoja na swali lililo hapo juu na utatakiwa kuandika 'YES' (NDIYO) au 'NO' (HAPANA) kwa kutumia Kiingereza ili kura yako ihesabiwe. Ikiwa utaandika 'YES' inamaanisha kuwa unakubali kwamba Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait wanapaswa kuwa na Sauti kuhusu masuala yanayowaathiri moja kwa moja.

### Nini itatokea kama watu wengi wanapiga kura YES (NDIYO)?

Ikiwa watu wengu wanapiga kura Yes kwa Sauti, ndipo Serikali itashauriana na Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait kukamilisha muundo na kuitisha sheria husika ili kuanzisha Sauti.

### Nini itatokea kama watu wengi wanapiga kura NO (HAPANA)?

Ikiwa watu wengu wanapiga kura 'No', hakuna kitu kitakachobadilika. Masuala yanayokabaliwa na Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait yataendelea. Kupiga kura 'No' kunamaanisha unapiga kura Hapana kwa Sauti, hakuna njia mbadala ya kuunga mkono Waaborijini na Wenyeji wa Visiwa vya Torres Strait katika Kura hiyo ya Maoni.

### Je, naweza kupata taarifa zaidi wapi?

habari  
zaidi

[www.lwb.org.au](http://www.lwb.org.au)

